JARIDA LA ROBO YA 2, OKTOBA-DESEMBA, 2023

# TANDAHIMBA DC




# JARIDA LA TANDAHIMBA DC

# YALIYOMO


3 Kamati ya ccm Wilaya kazini ukaguzi wa Miradi



4 Vijiji 17 kunufaika na Mradi wa Maji Mkwiti ifikapo Novemba 30, 2023.




30 HABARI PICHA



Bi. Shahara Mtanda ni mke wa mjasiriamali huyo, ameungana na mumewe katika kufanya shughuli ya kutengeneza viatu, amesema amejifunza kazi hiyo kiwandani hapo na sasa wanafanya kazi pamoja na kuingiza kipato cha familia.

34 KATUNI/VIBONZO



# Kamati ya ccm Wilaya kazini ukaguzi wa Miradi



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Tandahimba Mhe.Ismaili Mkadimba.amewataka wasimamizi wa Miradi kuongeza Juhudi katika kusimamia Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa Wilayani humo ili wananchi wapate huduma ambazo Serikali imekusudia kwa wakati.

ameyasema hayo Leo Oktoba 3, 2023 wakati Kamati ya Siasa Wilaya ya Tandahimba ilipofanya ziara ya ukaguzi wa Miradi mbambali ya Maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

Aidha, kamati ya Siasa Wilaya imeishukuru Serikali ya awamu ya Sita kwa kuendelea kutoa Fedha za Miradi katika Sekta za Afya, Elimu, Barabara, Maji na Nyinginezo ambapo kwa Pamoja zinalenga kuwahudumia na kuleta chachu ya Maendeleo kwa Wananchi wa Tandahimba.

Jumla ya Miradi yenye thamani ya zaidi ya Tsh. Bilioni 7.5 imekaguliwa na Kamati hiyo ukiwemo Mradi wa Vyumba vya Madarasa Shule ya Msingi Amani, Mabweni Mawili Shule za Sekondari Kitama na Luagala, Miradi ya Maji Kitama na Mkwiti, Pamoja Nyumba ya Mwaalimu (2-1) Shule ya Sekondari Litehu ,Ujenzi wa Zahanati Nachunyu pamoja na Machinjio ya Halmashauri.



# Vijiji 17 kunufaika na Mradi wa Maji Mkwiti ifikapo Novemba 30, 2023.




Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ( RUWASA) Wilaya ya Tandahimba Mhandisi. Antidius Muchunguzi amesema Serikali ilitoa Fedha kiasi Cha Tsh.Bilioni 6.5 kwa ajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Maji katika Kata Nne za Wilaya hiyo Mradi ambao utakamilika na Kuanza kutumika Mwezi Novemba, 2023.

Mhandisi Muchunguzi ameyasema hayo leo Oktoba 3,2023 wakati akisoma taarifa ya Maendeleo ya Ujenzi wa Mradi wa Maji Mkwiti na kuongeza kuwa Mradi huo ukikamilika unatarajia kuwahudumia wakazi wapatao 26,164 wa kata Nne za Mangombya, Ngunja, Litehu na Luagala .

“Jumla ya Vioski 45 vimejengwa katika vijiji 17 kwa ajili ya kuchotea maji na kuunganisha huduma ya maji katika taasisisi, Zahanati na Vituo vya Afya katika vijiji vyote 17 ambapo ongezeko hili litafanya watu wanaopata huduma ya maji Tandahimba kuongezeka kutoka asilimia 50 ya sasa hadi kufikia asilimia 60.2,” amesema Mhandisi Muchunguzi

Aidha, Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya wameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe Rais Dokta Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa (CCM) kwa kuufanya Mradi wa Maji Mkwiti kuwa miongoni mwa miradi inayoenda kuondoa kero ya maji kwa wananchi.



# “Wanafunzi zingatieni masomo” Mwenyekiti CCM



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tandahimba Mhe.Ismaili Mkadimba amewataka wanafunzi kuzingatia masomo ili wafikie malengo waliyojiwekea.

Ameyasema hayo wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Namikupa Oktoba 4,2023 mara baada ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Tandahimba ikiongozwa na Mwenyekiti Mhe.Ismaili Mkadimba kukagua mradi wa ujenzi wa bweni la Wasichana Shule ya Sekondari Namikupa

“Zingatieni masomo ili muweze kufikia malengo yenu,Serikali ya Awamu ya Sita imeboresha Miundombinu ya Elimu ili msome kwenye mazingira bora, jukumu lenu wanafunzi ni kuongeza bidii kwenye masomo,msijiingize kwenye mambo mengine ambayo yatawakatishia masomo yenu,” amesema Mhe.Mkadimba.

Aidha,amepongeza miradi iliyokamilika na kusistiza ianze kutoa huduma kwa wananchi lakini pia ameagiza miradi ambayo bado isimamiwe iweze kukamilika kwa wakati ili wananchi waweze kupata huduma.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala amesema maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Siasa ya CCM atayasimamia ili yatekelezwe kwa wakati na
wananchi wa Tandahimba waendelee kupata Maendeleo.

Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Tandahimba wamehitimisha ziara yao ya siku mbili Oktoba 4,2023 ambapo wametembelea na kukagua Jumla ya miradi yenye thamani ya zaidi ya Tsh.Bilioni 7.5



# Shilingi Bilioni 84.7 Kutekeleza Mradi wa maji Makonde



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) Wilaya ya Tadahimba wakiongozwa na Mhe.Ismaili Mkadimba wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa utekelezaji wa mradi wa Maji Makonde wenye thamani ya zaidi yaTsh.Bilioni 84.7 ambao utaongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

Pongezi hizo wametoa Oktoba 4,2023 wakiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambapo walitembelea mradi huo wa Makonde unaoendelea kutekelezwa Wilaya ya Tandahimba.

Akisoma taarifa ya Utekelezaji wa mradi huo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makonde Mhandisi Paulusi Nyagali kwa Kamati ya Siasa amesema kuwa kukamilika kwa
ujenzi wa mradi wa Makonde utaongeza upatikanaji
maji kutoka asilimia 63 iliyopo sasa hadi kufikia asilimia 90 ikiwa ni ongezeko la asilimia 27.
Aidha amesema kuwa mradi wa Makonde utanufaisha Halmashauri nne (4) ambazo ni Tandahimba,Newala Mji,Wilaya ya Newala na Nanyamba zikiwa na wakazi zaidi ya 670,000 ambao umelenga kuongeza uzalishaji maji kwa mita za ujazo 26,000 kwa siku kwa kutumia chanzo cha Maji Mitema ili kukidhi uzalishaji ambapo utakamilika Mwaka wa Fedha 2024/2025
Miradi mingine iliyotembelewa na Kamati ya Siasa siku ya pili ya ziara ni Mradi wa Shule ya Msingi Nandonde, Bweni la Wasichana Shule ya Sekondari Namikupa, ujenzi wa madarasa manne Shule ya Msingi Milidu,Zahanati ya Chikongo,Kituo cha Afya Maheha,Zahanati ya Mnazimmoja,mradi w maji Lipalwe,ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari Mahuta,ujenzi wa Shule ya Sekondari Mndumbwe,Shule ya Msingi Mambamba ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Machedi na Shule ya Msingi Mjimpya .



# Dc Tandahimba akutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa



Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala amekutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa wa Wilaya ya Tandahimba kuimarisha Mahusiano na Ushirikiano ili kuendelea kuhamasisha wananchi katika shughuli za Maendeleo.

Akizungumza na Viongozi hao Oktoka 6,2023 Dc Sawala amesema wameruhusiwa kufanya mikutano lakini ni jambo jema kutoa taarifa mapema kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama kwenye eneo la Mkutano.

“ Tuendelee kuimarisha mahusiano na.ushirikiano huku tukitambua wote tunajenga nyumba moja ya kuwaletea wananchi wa Tandahimba Maendeleo,Siasa za kistaarabu ni nzuri mnashindana kwa hoja ,” amesema Dc Sawala.

Kwa upande wa Viongozi wa Vyama vya siasa wamepongeza hatua ya Mkuu wa Wilaya kukutana nao na wameiomba Serikali ya Wilaya hususan Jeshi la Polisi kutoa ushirikiano wanapohitaji ulinzi wa Jeshi la polisi kwenye Mikutano yao ya hadhara.

Naye Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Tandahimba SP.Kulwa Biteme amewahakikishia Viongozi wa Vyama vya Siasa ulinzi na usalama wakiwa kwenye mikutano yao ya hadhara ambapo amesema muhimu kuzingatia taratibu miongozo na sheria za kufanya mikutano ya hadhara.



# Kamati ya Siasa Mkoa wa Mtwara yaridhishwa na Miradi ya maendeleo Tandahimba.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mtwara Mhe. Said Nyengedi amewaongoza wajumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Mtwara katika ziara ya kukagua Miradi ya Maendeleo inayopo na inayotekelezwa Wilaya ya Tandahimba.

Akizungumza wakati akikagua Mradi wa Maji Lipalwe wenye gharama ya Tsh.Milioni 553.3 Mhe.Nyengedi ameipongeza Serikali kwa kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) kwa Vitendo na Wananchi wananufaika na Miradi hiyo.

Mradi wa Maji Lipalwe ambao umekamilika na Wananchi wapatao 2981 wa Vijiji vya Lipalwe A" na B" wanatumia Maji hayo ambapo wanufaika hasa akina mama watatumia muda mwingi kwenye Uzalishaji Mali badala Kutafuta Maji.

Kwa Upande wake Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa Miradi Mikubwa inayoendelea kutekelezwa Wilayani humo akiahidi kuendelea kuisimamia vyema ili ilete tija kwa wananchi.

Miradi mingine iliyokaguliwa na Kamati ya Siasa Mkoa ni pamoja na Mradi wa maji Lipalwe, Ujenzi wa Sekondari mpya ya Mahuta, Mradi wa usambazaji umeme vijijini (REA), na Uzinduzi wa utoaji wa huduma za afya kwa wananchi katika zahanati ya Mnazimmoja.



# Viongozi ngazi ya Kata wanatakiwa Kuhamasisha usafi wa mazingira kwenye maeneo yao



Viongozi ngazi ya Kata Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba wametakiwa kuhamasisha Jamii ujenzi wa vyoo bora na usafi wa mazingira katika maeneo yao ili kuepuka magonjwa yatokanayo na uchafu wa mazingira.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Raphael Mputa kwenye kikao kazi kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri amesema ni jukumu la viongozi kusimamia na kuhimiza usafi wa mazingira na ujenzi wa vyoo bora kwa Jamii.

“ Viongozi mkazingatie maelekezo ya wataalamu waliyowapa,mkasimamie na mtoe elimu kwa wananchi katika mikutano yenu mnayofanya ili kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora na usafi wa mazingira sambamba na kufanya kazi zenu kwa uadilifu” amesema Ndg.Mputa.

Kwa upande wa Wawezeshaji wamesisitiza kuwa mkakati wa pamoja ni kusimamia na kuhimiza usafi wa mazingira na kila kaya iwe na vyoo bora na vibuyu chirizi kwa ajili ya kunawa mikono ili kuendelea kuimarisha afya bora kwenye jamii.

Aidha, wawezeshaji wameeleza kuwa takwimu sahihi zitachukuliwa kila robo ya Mwaka ambapo Wenyeviti wa Vitongoji watapita katika kila kaya kuona hali halisi na kuchukua taarifa za kaya husika ambapo kijiji kitakachofanya vizuri kitapewa fedha na Mradi wa WASH wa Lipa kwa matokeo (P4R) ambazo watazitumia katika shughuli zao za Maendeleo kwenye kijiji chao.

Kikao hicho kilianza Oktoba 12,2023 kimehitimishwa leo Oktoba 13,2023 ambapo kimehudhuriwa na Maafisa Tarafa,Watendaji Kata,Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa vitongoji



# Mnada wa kwanza wa Korosho wafanyika Tandahimba



Chama Kikuu cha Ushirika Tandahimba na Newala(TANECU) kimefanya Mnada wa kwanza wa zao la Korosho kwa Msimu wa kilimo Cha Korosho 2023/2024 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ambapo Korosho imeuzwa kwa Bei ya juu ya Tsh.2050 na Bei ya Chini Tsh.1950 Kwa kilo moja.

Mwenyekiti wa TANECU Karim Chipola amewasisitiza Wakulima kuziandaa Korosho kwa Ubora kabla ya kuzipeleka ghalani.

“Ukipeleka Korosho Mbichi ghalani inaharibu soko na kushusha Bei, niwasisitize endeleeni kuzikausha na kuepuka kuongeza vitu ambavyo siyo Korosho “ Chipola

Akisoma hali ya Ukusanyaji wa Korosho kwa Mnada wa kwanza Meneja wa TANECU Mohamed Nassoro amesema Jumla ya Tani 7752 zimekusanywa ambapo kati ya hizo Tandahimba imekusanya Jumla ya Tani 5981.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba,Kaimu Katibu Tawala Wilaya hiyo Francis Mkuti ameishukuru Serikali kwa kutoa Pembejeo kwa wakulima Bure hali iliyopelekea Uzalishaji wa Korosho kuongezeka .



# Shirika la Medea latambulisha Mradi wa Sauti zetu Tandahimba



Shirika lisilo la Kiserikali la Medea Tanzania limeutambulisha Mradi wa Sauti Zetu ambao utafanyika kwa Miaka Miwili kuanzia Mwaka 2023 hadi 2025 katika Wilaya ya Tandahimba ambao utafanyika katika Kata ya Tandahimba na Milongodi .

Akiutambulisha mradi huo ngazi ya Wilaya leo Oktoba 25,2023 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Mkuu wa Wilaya Mratibu wa Mradi Ndg.Alpha Kimweri amesema mradi huo utatoa elimu kwa Jamii ili kujenga Uelewa wa Madhara ya Ndoa za Utotoni.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Tawala Wilaya ya Tandahimba Ndg.Juma Lusasi akizungumza kwenye kikao hicho amewapongeza kuleta mradi huo ili kujenga uelewa kwa Jamii madhara ya Ndoa za Utotoni huku akiwasisitiza kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.



# Wadau wa korosho Tandahimba na Newala wakutana kuweka mikakati ya kudhibiti ubora wa zao hilo.



Wadau wa Korosho Wilaya ya Tandahimba na Newala wameweka mikakati ya kudhibiti ubora wa Korosho ili kuongeza thamani ya bei kwa wanunuzi wanaokuja kununua korosho hizo

Akifungua kikao hicho jana Oktoba 26,2023 Katika ukumbi wa mikutano wa Wilaya ya Newala, Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe.Alhaji Mwangi Rajabu Kundya amesema thamani ya korosho inapoongezeka wanufaika ni wakulima wa zao hilo

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala amewasistiza maafisa Ugani,Maafisa Ushirika na Viongozi wa Vyama vya Ushirika kuendelea kutoa elimu kwa Wakulima ya ukaushaji wa korosho na kuhifadhi katikaviwango vinavyotakiwa huku akiwataka watunza maghala kusimamia ubora wa korosho kwa kuzingatia vipimo vya unyevu kabla ya kuingiza ghalani.

Katika hatua nyingine viongozi hao wakiwemo wa vyama vya ushirika (AMCOS) na watunza Maghala kwa pamoja wameahidi kusimamia kwa weledi majukumu yao pamoja na kuzingatia maelekezo waliyopewa ili kuendelea kulinda ubora wa korosho hizo.

Mpaka sasa Wilaya ya Tandahimba inaongoza kwa uzalishaji wa korosho bora nchini Tanzania



# Kamati ya lishe ya Wilaya yajadili taarifa ya utekelezaji wa afya za lishe robo ya kwanza 2023/2024



Kamati ya Lishe Wilaya ya Tandahimba leo Novemba 6,2023 imejadili utekelezaji wa afua za lishe kwa kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba,2023

Akizungumza kwenye kikao hicho kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Raphael Mputa amesema ili jamii iweze kufanya shughuli za kimaendeleo inahitaji kuwa na afya bora hivyo amesistiza elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu

***" Elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu afya na lishe sambamba na kuyatekeleza yale ambayo tumekubaliana katika kikao hiki ," amesema Mputa***

Aidha katika kikao hicho Divisheni na vitengo ziliwasilisha taarifa za utekelezaji wa afua za lishe kwa kwa kipindi cha robo ya kwanza ambapo Kamati zilijadili taarifa hizo .

Naye Mganga Mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Dr.Grace Paul amesema timu za wataalamu wa afya na lishe wameendelea kutoa elimu kwa jamii katika Kata na Vijiji

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kupitia kamati ya lishe na viongozi mbalimbali wamekuwa Mstari wa mbele katika kuhamasisha na kutoa Elimu ya lishe ili keuepuka Udumavu na kujenga Jamii yenye Afya Bora.



# NMB Tandahimba yakabidhI Madawati, Stuli Mabati Yenye Thamani ya Tsh.Milioni 63.9.






Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala amepokea mabati 369,madawaati 390 na stuli za maabara 100 zote zikiwa na thamani ya Tsh Milioni 63.9 kutoka Benki ya NMB tawi la Tandahimba ikiwa ni mchango wao kwa sekta ya elimu kuunga juhudi za Serikali katika sekta hiyo.

Akizungumza Novemba 7,2023 kwenye Hafla fupi ya makabidhiano ya vifaa hivyo yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri na kuhudhuriwa na Wakuu wa Idara na watumishi Dc Sawala ameipongeza benki ya NMB kwa vifaa hivyo ambapo amesema vitasaidia katika ujifunzaji na ufundishaji katika shule hizo.

“ Nawapongeza sana Benki ya Nmb kwa mchango huu wa madawati,mabati na stuli za maabara ambazo zinakwenda kupunguza uhaba kwenye shule zetu,wito kwa taasisi nyingine kuiga mfano wa NMB wa kurudisha kwa jamii,ili kuendelea kuunga juhudi za Serikali katika Sekta ya Elimu” amesema Dc Sawala.

Kwa upande wake Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini Ndg.Faraja Ng’ingo akikabidhi vifaa hivyo amesema kuwa benki hiyo imekuwa na utaratibu wa kurudisha faida ya asilimia 1 wanayoipata kwa jamii ambapo wanachangia katika sekta ya Elimu na Afya kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii inayowazunguka.




“ Tunatambua juhudi za Serikali ya awamu ya sita ya kusimamia upatikanaji wa Elimu bora kwa nguvu zote,hatuna budi kuipongeza Serikali kwa hilo na sisi kama wadau tunao wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za Maendeleo kwani jamii imeifanya Benki ya NMB kuwa hapa tulipo,” amesema Meneja wa Kanda

# CMT Tandahimba Kazini Kutembelea Miradi.



Timu ya Menejimenti (CMT) ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ACI. Mariam Mwanzalima Novemba 27, 2023 imefanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya Maendeleo .

Akizungumza na Fundi viongozi ambao aliwakuta katika miradi hiyo wanayoitekeleza Mkurugenzi Mtendaji amewasistiza kukamilisha miradi kwa wakati na ubora ili ilete tija sambamba na kuzingatia mikataba yao.

Miradi iliyotembelewa na CMT ni Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi shikizi Michenjele,Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi shikizi Mihambwe Ujenzi wa Shule mpya mahuta(Makondeni Sekondari), Ujenzi wa Shamba darasa la ufugaji wa viumbe maji Kata ya Chaume na Ujenzi wa bweni la wavulana Shule ya Sekondari Luagala.

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo
ambayo ipo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji.



# Kamati Ya Fedha yakagua Miradi yenye thamani ya zaidi ya Tsh.bilioni 1.1 , yasisitiza ikamilike kwa wakati.



Kamati ya Fedha Utawala na Mipango Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Novemba 9, 2023 imekagua Miradi 10 ya Maendeleo katika Sekta ya Afya, Elimu na Uvuvi yenye Jumla ya Tsh.Bilioni 1.1 inayotekelezwa katika Wilaya hiyo.



Akizungumza wakati wa ukaguzi huo Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mhe. Baisa Baisa amesema Serikali inatoa Fedha nyingi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hivyo ni jukumu la Viongozi na watumiaji wa Miradi hiyo kuitunza ili idumu kwa Muda mrefu.

Aidha, Mhe.Baisa amesisitiza Wakandarasi walipwe kulingana na kazi wanazozifanya ili kuongeza Kasi na utendaji wa kazi Kwa makini zaidi ikilinganishwa na wanapopewa Fedha kiasi kabla ya Mradi kukamilika.

Kwa Upande wake Diwani wa Kata ya Mnyawa ambae ni Mjumbe wa Kamati hiyo ya Fedha Mhe. Rashid Njawala amesisitiza maelekezo ya kuboresha yanayotolewa na Kamati yafanyiwe kazi ili watakapokagua mara nyingine wakute miradi ikiwa katika Ubora zaidi.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Robert Mwanawima ameahidi kuyafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na Kamati yenye lengo la kuboresha miradi hiyo huku akisisitiza kuendelea kufanya ufuatiliaji kupitia Menejimenti ya wataalamu katika kutekeleza Miradi hiyo kwa ufanisi.

# Miradi yote ambayo Serikali imetoa Fedha lazima ikamilike” Ded Mwanzalima



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ACI.Mariam Mwanzalima amefanya Ziara ya kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri hiyo na kutoa maelekezo kwa viongozi wanaosimamia Ujenzi huo kuhakikisha inakamilika katika Ubora na Kwa wakati.



DED Mwanzalima ameyasema hayo Novemba 12, 2023 alipotembelea katika nyumba ya Mwalimu 2(1) yenye Gharama ya TSH.Milioni 95 , Shule ya Msingi Litehu na Shule ya Msingi Liponde na kuongeza kuwa yeyote atakayesababisha Mradi kusua sua atawajibishwa kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa.

Aidha, amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa Fedha za Maendeleo kwa Wananchi wa Tanda-

# Mkandarasi Yuko Site Ujenzi WaShamba Darasa la Ufugaji wa Viumbe Maji Tandahimba,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Joshua Mgoli Septemba 15, 2023 ametembelea na kukagua Ujenzi wa Miundombinu ya Shamba Darasa la Ufugaji wa Viumbe Maji linalojengwa katika Kata ya Chaume .



Ujenzi wa Miundombinu hiyo utagharimu Tsh.Milioni 125.8 Fedha kutoka Serikali kuu ambapo tayari Mkandarasi ameanza kazi ya Ujenzi huo unaotarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Machi, 2024.

Aidha, Mradi huo unatarajia kuwanufaisha wananchi ambao watafundishwa kuandaa mashamba Yao ya Ufugaji wa Viumbe Maji wakiwemo Samaki ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi.



# Watumishi Tandahimba wapatiwa Mafunzo ya Mfumo wa Pepmis na Pipmiss



Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba wamepatiwa mafunzo ya mfumo wa kielektroniki wa kujisajili kwenye mfumo wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma( PEPMIS/PIPMIS)

Mafunzo hayo yamefanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ambapo mwezeshaji Ndugu.Raphael Mputa amesema kwenye mfumo huo watumishi wote watajaza taarifa zao za kiutumishi na fomu za upimaji wa kazi zao .

Aidha mafunzo hayo yameanza leo Novemba 28,2023 kwa watumishi wote wa Ofisi kuu ambapo pia mafunzo hayo yatatolewa kwa watumishi wote waliopo ngazi ya Kata na Vijiji kwenye Tarafa zao.



# Kamati ya Siasa Tandahimba yapongeza utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo



Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tandahimba ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya Mhe. Ismaili Mkadimba imefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya Maji inayotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

Ziara hiyo imefanyika leo Novemba 29,2023 ambapo Kamati imetembelea chanzo cha Maji Mitema na kuona kazi zilizopangwa kufanyika kuongeza uzalishaji wa maji ili wananchi wa Tandahimba waendelee kunufaika na chanzo hicho,Mradi wa maji Mkwiti unaotekelezwa na RUWASA na Mradi wa Maji wa Miji 28 wenye gharama ya Tsh.Bil 84.7 unaotekelezwa na Makonde.

wakazi 26,164.wa RUWASA Wilaya ya



Aidha Mwenyekiti wa CCM Mhe.Mkadimba ameagiza kuongeza kasi na usimamizi katika utekelezaji wa mradi wa Mkwiti uweze kukamilika ili urahisishe upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa vijiji 17 ambavyo vina jumla ya

Kwa upande wake Meneja Tandahimba Injinia Antidius Muchunguzi akiwasilisha taarifa yake ya mradi wa maji Mkwiti amesema utekelezaji unaendelea ambapo kazi zingine zilizopangwa kufanyika zimekamilika.

# Wadau Waweka Mikakati Ya Utoaji Wa Taarifa Za Ukatili.

Kuelekea katika Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga ukatili wadau wameweka mikakati ya utoaji wa taarifa sahihi za matukio ya ukatili katika jamii ili kupunguza vitendo hivyo.

Akifungua mafunzo ya siku moja Ndugu Aloyce Massau kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kwa wadau 46 walioshiriki Novemba 30,2023 kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri amesema utoaji wa taarifa sahihi za matukio ya ukatili unaweza kupunguza vitendo hivyo kwa Jamii .




> ***"Tukawe mabalozi wazuri kwenye jamii kwa kutoa elimu ili jamii iweze kutoa taarifa sahihi za vitendo vya ukatili vinavyofanyika katika maeneo yao na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wahusika wanaofanya ili kupunguza vitendo hivyo, " amesema Massau***




Kwa upande wake Mratibu wa Shirika la Faidika Wote Pamoja( FAWOPA) Ndugu Justine Kabelege ambaye pia ni mratibu wa mradi waTamaduni zetu Kesho yetu ambao unatekelezwa katika Kata nne za Tandahimba amesema wadau wameweza kuibua matukio mbalimbali ya ukatili kama vile Taraka holela, Utelekezaji wa Wa toto, Matukio ya Ubakaji na Matukio ya kupigwa kwa Wanawake, ambapo wameweka mkakati wa kushughulikia matukio ya ukatili ikiwa pamoja na kuboresha mawasiliano ili kukuza muamko wa utoaji wa taarifa na ushirikiano.

# Naibu Waziri wa Kilimo Mhe.silinde azindua Mfumo wa upimaji wa mazao Kidigitali



Naibu Waziri wa Kilimo Mhe.David Silinde amezindua mfumo wa upimaji wa mazao ya wakulima kupitia mizani ya kidigitali iliyounganishwa na mfumo wa usimamizi wa vyama vya ushirika ( MUVU).

Uzinduzi huo umefanyika leo Disemba 5,2023 kwenye eneo la maghala ya Chama Kikuu cha Ushirika Tanecu ambapo Mhe. Silinde ameagiza vyama vyote vya ushirika kutumia mizani ya kidigitali sambamba na kuhakikisha mtandao huo un apatikana vijijini kwa uhakika kwenye amcoss ili wakulima wapate huduma kwa ufanisi.

*"Nimezindua rasmi mfumo huu na zoezi la usambazaji wa mizani ya kidigitali ambapo itakwenda kupunguza malalamiko ya wakulima ya kupunjwa kwa kilo za mazao yao wanapopeleka sokoni na mfumo huu utaongeza ufanisi na utendaji kwenye vyama vya ushirika," amesema Mhe.Silinde.*

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe.Kanali Patrick Sawala amesema mfumo huu utamsaidia mkulima kila atakapopima kupata ujumbe kwenye simu yake ambao utasaidia kupunguza malalamiko na ametoa wito kwa wataalamu kutoa elimu zaidi

Aidha kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Tandahimba Mhe.Katani Katani ameiomba Serikali kuchukua hatua za Kisheria kwa wanunuzi wanaotaka kuhujumu Korosho ya Tanzania.



# Dc Sawala aongoza Watumishi na Wananchi kufanya usafi Hospitali ya Wilaya



Kuelekea Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe Kanali Patrick Sawala amewaongoza Watumishi na Wananchi kufanya Usafi wa Mazingira katika Hospitali ya Wilaya ya Tandahimba.

Akizungumza leo Disemba 8,2023 mara baada ya kukamilisha kufanya usafi,Dc Sawala amewapongeza wote walioshiriki kwenye zoezi hilo la usafi na kuwasistiza kuendelea kudumisha Amani na Umoja ambayo ni nguzo ya Maendeleo .

Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru Wa Tanzania Bara ni Disemba 9,2023 ambapo Kiwilaya yataadhimishwa kwa bonanza la michezo mbalimbali na kisha kukamilisha kwa kufanya Mdahalo kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ambapo pia Mgeni rasmi atakabidhi zawadi mbalimbali kwa wanafunzi washindi wa uandishi wa Insha.



# Wananchi Tandahimba waipongeza Serikali Miaka 62 ya Uhuru



Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba leo Disemba 9,2023 wameshiriki mdahalo wa Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara ambapo wameipongeza Serikali kwa kuboresha sekta mbalimbali nchini.

Wakizungumza kwenye mdahalo huo uliofanyika kwenye ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ukiongozwa na Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba ambaye ni Katibu Tawala Ndugu .Rashidi Shabani, na kuhudhuriwa na Wazee maarufu,viongozi wa vyama vya siasa,viongozi wa dini,Kamati ya Usalama ya Wilaya,Timu ya Menejimenti,Wakuu wa taasisi,Watumishi na wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Tandahimba

Katika Mdahalo huo wachangia mada wameeleza Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilipotoka katika sekta zote ,ilipo sasa ambapo wamesema Maendeleo yanaonekana kwa macho na inapoelekea kimaendeleo, pia wametoa mapendekezo yao kwa Serikali kuendelea kusimamia mila,desturi na tamaduni ili kulinda na kuzingatia maadili ya kizazi kilichopo na kijacho .

Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara hufanyika kila Mwaka ambapo Kitaifa Mwaka huu yamefanyika Mkoani Dodoma chini ya kauli mbiu "Umoja na Mshikamano ni chachu ya Maendeleo ya Taifa letu"



# Mwenyekiti Wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ahudhuria Mkutano Wa Cop 28-Dubai




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Mhe.Baisa amehudhuria Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia nchi ( Climate Change COP 28) Unaofanyika Dubai.

Katika mkutano huo Mhe. Baisa , ameshauri uwezekano wa miti ya mikorosho kuingizwa kwenye biashara ya hewa Ukaa ( Carbon Business) jambo ambalo litawapatia kipato wakulima wa Korosho.

# Madiwani Kisarawe wafanya ziara Tandahimba kujifunza zao la Korosho



Madiwani na baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe wakiwa wameongozana na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Mhe.Fatma Nyangasa wamefanya ziara ya kujifunza Uzalishaji wa kilimo bora cha Korosho Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

Baada ya kuwasili katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Disemba 14,2023 Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala aliwasomea taarifa fupi ya Wilaya kisha wataalamu waliwasilisha mada muhimu za uzalishaji wa Korosho.

Wakiwa Tandahimba wametembelea kitalu cha miche ya korosho Kata ya Tandahimba,Shamba la Mikorosho Kitama,kujifunza mfumo wa stakabadhi ghalani Chama cha msingi Namunda na Kiwanda cha Ubanguaji Korosho TDC.

Aidha akizungumza kwa niaba ya Timu ya Wilaya ya Kisarawe Dc Nyangasa amepongeza juhudi zinazofanywa na Serikali katika zao la Korosho ambapo pia aliwapongeza wataalam wa Halmashauri ya

Tandahimba wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti kwa kufanikisha ziara yao.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Mhe. Rehema Liute amewapongeza kwa kuchagua Halmashauri ya

Wilaya ya Tandahimba kuja kujifunza ambapo amesema kuwa ziara yao ikalete matokeo chanya kwenye Halmashauri yao.



# Dc Sawala akabidhi Pikipiki kwa Maafisa Ugani Tanecu




Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe Kanali Patrick Sawala amekabidhi pikipiki 13 zenye thamani ya Tsh.Mil.30.4 kwa Maafisa Ugani wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Tanecu.

Akikabidhi pikipiki hizo leo Disemba 15,2023 Dc Sawala amewasistiza Maafisa Ugani kuwafikia wakulima kwenye maeneo yao na kuwapa elimu ili kuongeza uzalishaji wenye tija.

***"Pikipiki hizi zikafanye kazi iliyokusudiwa ambayo ni kuwafikia wakulima kwenye maeneo yao na kuwapa elimu huku mkizingatia Sheria za Usalama barabarani mnapoendesha vyombo hivyo vya moto," amesema Dc Sawala.***

wa Newala.
Kwa upande wake Meneja Mkuu wa Tanecu Mohamed Mwing'uku amesema kuwa pikipiki hizo zimetolewa kwa Maafisa Ugani 13 ambapo saba (7) wa Tandahimba na sita (6)

Aidha kwa upande wao Maafisa Ugani wameshukuru na kuahidi kutumia pikipiki hizo kwa kazi iliyokusudiwa.



# Rc Mtwara apongeza ujenzi wa Miradi ya Elimu Sequip na Boost Tandahimba.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas leo Desemba 20, 2023 ametembelea na kukagua Maendeleo ya Ujenzi wa Shule ya Sekondari Mahuta na Shule ya Msingi Mambamba na kuwapongeza viongozi kwa usimamizi Mzuri huku akiwataka Wananchi kutumia fursa hiyo kuwahimiza wanafunzi kwenda Shule mara baada ya Shule hizo Mpya Kufunguliwa.

*"Uwezekano wa kuwaleta wanafunzi mwakani upo, hivyo nitoe Rai kwa Wazazi kuhakikisha wanawaleta wanafunzi ili miundombinu hii ikalete maana iliyokusudiwa" Kanal Abbas*

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuleta Miradi yenye tija kwa Wananchi wa Tandahimba.
Kwa Upande wao Wananchi wa Mahuta na Mambamba wametuma salamu za kumshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali watoto wao kwa kuboresha Miundombinu ya Elimu.

Ujenzi wa Shule ya Sekondari Mahuta umegharimu Tsh.Milioni 560.6 fedha kutoka Serikali kuu kupitia Mradi wa SEQUIP sambamba na Shule ya Msingi Mambamba inayogharimu Tsh.Milioni 331.6 ikiwa ni fedha kutoka Serikali kuu kupitia Mradi wa BOOST inatarajiwa kuanza kutumika ifikapo Januari 2024 .



# “Wananchi limeni na mazao mengine” Rc Kanali Abbas



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas amewaasa Wananchi wa Tandahimba kutokutegemea zao moja la Biashara ambalo ni Korosho na badala yake walime na mazao mengine yenye tija ili kukuza uchumi wao.

Kanali Abbas ameyasema hayo Leo Desemba 20, 2023 wakati akizungumza na wananchi mara baada ya kukagua Shule ya Msingi Mambamba.

“Niwasisitize wakulima wetu kuwa mbali na Korosho limeni mazao Mengine Mbadala yaliyoelekezwa ikiwemo Mbaazi na Ufuta ili kwa Mwaka Mzima kuwe na shughuli za uzalishaji Mali “Kanali Abbas.

Sambamba na hilo Kanali Abbas amewaasa Wananchi kuchukua Tahadhali na kujikinga na Magonjwa ya Mlipuko hasa kipindi hiki Cha Mvua nyingi pamoja nakuepuka kuishi mapondeni ambako Mkondo wa Maji unapita.



# “Tumepiga hatua kubwa Sekta ya maji Tandahimba “Dc Sawala.



Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala amesema Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mageuzi makubwa katika kutoa huduma za Msingi kwa Jamii ikiwemo maji ambapo Wilaya hiyo imenufaika na Miradi ya maji inayotekelezwa kwa Wananchi ikilinganishwa na miaka ya Nyuma.

DC Sawala ameyasema hayo Leo Desemba 21, wakati akifungua Mkutano wa Nusu Mwaka wa Wadau wa Maji uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri hiyo.

“Hali ya upatikanaji wa Maji katika Wilaya yetu kwa sasa hauwezi kulinganisha na Miaka Miwili iliyopita ambapo ilikuwa Chini ya 20% lakini kwa sasa inakwenda mpaka 51% ni jitihada kubwa zimefanywa na zinaendelea kufanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita” DC Sawala

Sambamba na hilo DC Sawala amewapongeza Viongozi wa RUWASA na MAKONDE kwa kuendelea kusimamia vyema upatikanaji wa Maji kwa Wananchi pamoja na Miradi Mikubwa ya Maji inayoendelea kujengwa Tandahimba huku akiwaasa Jumuiya za Maji kuhakikisha zinasimamia vyema ukusanyaji wa mapato ili Miradi hiyo ya Maji iendelee kujiendesha.

Kwa Upande wake Meneja wa RUWASA Wilaya ya Tandahimba Mhandisi Antidius Muchunguzi amesema mpaka sasa Wananchi 152,658 kati ya wananchi 299,073 wanapata huduma ya maji sawa na 51% na kuongeza kuwa ifikapo Mwaka 2025 Hali ya upatikanaji wa Maji itafikia 90%.

# Jeshi la Polisi lateketeza Dawa za Kulevya zaidi 507.9 Kg Tandahimba.



Jeshi la Polisi Wilaya ya Tandahimba Leo Desemba 28,2023 limeteketeza kwa moto Dawa za Kulevya aina ya bangi zenye uzito wa Kilogram 507.9 pamoja na Heroin gram 3.89 katika Dampo la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na kushuhudiwa na viongozi mbalimbali Wa Wilaya hiyo.

Akizungumza wakati wa kuteketeza Dawa hizo Salome Mbonile ambae ni Kaimu Kamishna Msaidizi Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya amesema pamoja na kutekeza Dawa hizo amewataka Wananchi kutoa taarifa na ushirikiano kwa Mamlaka ya Dawa za Kulevya ili kuwakamata wanaojihusisha na Dawa hizo waweze kuchukuliwa hatua za Kisheria.

Pamoja na Dawa hizo jeshi la Polisi Wilaya hiyo limemwaga jumla ya Lita 75 za Pombe ya kienyeji maarufu kama Gongo ambapo watuhumiwa walifikishwa mahakamani na Sheria zimechukuliwa dhidi yao.



# HABARI PICHA




*Oktoba 24, 2023*
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ACI.Mariam Mwanzalima akikagua mradi wa ujenzi wa Bweni la Wasichana Shule ya Sekondari Luagala wenye gharama ya Tsh.Milioni 150 na mradi wa Ujenzi wa nyumba ya Walimu (2 in1) Shule ya Sekondari Litehu Modern wenye gharama ya Tsh.Milioni 95 ambapo miradi yote ipo kwenye hatua ya ukamilishaji.*
*#Tandahimba tumejipanga, kazi zinaendelea*



***Oktoba 26,2023***
***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ACI.Mariam Mwanzalima alipotembelea na kukagua Maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Chuo Cha Ufundi VETA kilichopo Kitama ambapo amewataka Wahandisi kuongeza kasi katika utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa wakati***

*“Serikali imeendelea kuboresha mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji ni wajibu wenu wanafunzi kusoma kwa bidii ili mfikie malengo mliyojiwekea,hakuna njia mbadala ya kufikia malengo yako bila kusoma kwa bidii,” Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe.Kanali Patrick Sawala*





*“Mkishirikiana nyie viongozi kuanzia ngazi ya Vijiji  hadi Kata mtafika mbali kwakuwa mtaweka mikakati mizuri ya Maendeleo kwenye Kata yenu hususan ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ya vijiji na kuwawezesha wananchi  kiuchumi hususan vijana,” Mkurugenzi Mtendaji HaACI. Mwanzalima.*


#TumewasikiaTumewafikia
Maelezo
Kiwanda cha Kushona Viatu
vya Ngozi na Shanga
Tandahimba - Mtwara.
Bwana Muhib Hatib Nahama mkazi wa Tandahimba na Mjasiriamali mwenye ulemavu amenufaika na mkopo wa asilimia kumi wa halmashauri kiasi cha shilingi milioni 8 zilizomuwezesha kufungua kiwanda kidogo cha kutengeneza viatu vya ngozi na shanga ambapo shilingi milioni 6 zilitumika kununulia mashine mbalimbali za ushinaji na shilingi milioni 2 kwa ajili ya malighafi


#TumewasikiaTumewafikia
Maelezo
Kiwanda cha Kushona Viatu
vya Ngozi na Shanga
Tandahimba - Mtwara.

# #TumewasikiaTumewafikia

## Kiwanda cha Kushona Viatu vya Ngozi na Shanga

Tandahimba - Mtwara.





Namshukuru Mungu kuwa kila ninapolala nikiamka najua naenda wapi na nafanya nini, sasa hivi nafanya kazi, mwanzoni nilikuwa nashona tu viatu na kandambili, anamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kusimamia na kuhakikisha asilimia kumi za mapato ya ndani kwa ajili ya Vijana, Wanawake na Makundi Maalum kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba inapatikana.


# #TumewasikiaTumewafikia

## Kiwanda cha Kushona Viatu vya Ngozi na Shanga

Tandahimba - Mtwara.








Bi. Shahara Mtanda ni mke wa mjasiriamali huyo, ameungana na mumewe katika kufanya shughuli ya kutengeneza viatu, amesema amejifunza kazi hiyo kiwandani hapo na sasa wanafanya kazi pamoja na kuingiza kipato cha familia.

# KATUNI/VIBONZO







SINA HELA
CHAGUA KWENDA GEREJI AU NIKUFUNGULIE KIBANDA CHA KUUZA FIRIGISI
BABA! SERIKALI INATOA ELIMU BILA ADA, MADARASA YAPO YA KUTOSHA KWA NINI NISIANZE KIDATO CHA KWANZA!?
KUMBE!
HAYA ONGOZA NJIA NIKANUNULIE MAHITAJI, UKARIPOTI UPESI KABLA YA HIYO TAREHE 31 JANUARI
YEES! MAMBO SI HAYO
NDOTO YANGU ITATIMIA


VIBALI VYA UJENZI!
YES.
YA HALMASHAURI
VINAEPUSHA UJENZI HOLELA

Tandahimba District Council-TDC

tandahimbadistrictcouncil

www.tandahimbadc.go.tz

TDC ONLINE TV

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA